## SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU (HAKI NA FURSA) NAM. 9 YA MWAKA 2006 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA MASHARTI YANAYOHUSIANA NA WATU WENYE ULEMAVU NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

### MPANGILIO WA VIFUNGU


VIFUNGU MAELEZO

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Ufafanuzi.

SEHEMU YA PILI
UANZISHWAJI, USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA BARAZA

3. Uanzishwaji wa Baraza.

4. Muhuri na Nembo ya Baraza.

5 Muundo wa Baraza.

6. Kazi za Baraza.

7. Uwezo wa Baraza.

8. Sifa za Mwenyekiti.

9. Makamu Mwenyekiti.

10. Posho la Wajumbe.

11. Kamati za Baraza.

12. Muda wa Wajumbe wa Baraza.

13. Kusita kuwa Mjumbe.

14. Kukasimu kazi za Baraza.

15. Mwenendo wa Baraza.

16. Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

17. Muda wa Wajumbe wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

18. Kazi za Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

19. Mwenendo wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

20. Katibu Mtendaji wa Baraza.

21. Sifa za Katibu Mtendaji.

22. Kazi za Katibu Mtendaji.

23. Sekretarieti.

24. Wafanyakazi wa Baraza.

**SEHEMU YA TATU**
**USAJILI WA WATU MWENYE ULEMAVU NA JUMUIYA ZA WATU WENYE ULEMAVU**

25. Taratibu za usajili.

26. Daftari la kumbukumbu.

27. Sifa za Kusajiliwa.

**SEHEMU YA NNE**
**HAKI NA FURSA**

28. Haki na fursa.

29. Ufikiaji.

30. Wajibu wa kulinda haki za Watu Wenye Ulemavu.

31. Kuondoa Ubaguzi na udhalilishaji.

## SEHEMU YA TANO
## UKONDOESHAJI NA UJUMUISHAJI


32. Ukondoeshaji na ujumuishaji.

33. Miundombinu Rafiki.


## SEHEMU YA SITA
## MFUKO WA MAENDELEO YA WATU WENYE ULEMAVU


34. Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu.

35. Uendeshaji na Usimamizi wa Mfuko.

36. Vyanzo vya Mfuko.

37. Malengo ya Mfuko.

38. Ukaguzi wa Mfuko.


## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA


39. Vyanzo vya Fedha.

40. Bajeti ya Baraza.

41. Hesabu na Ukaguzi.


## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU


42. Kumficha Mtu Mwenye Ulemavu.

43. Taarifa ya Uongo.

44. Kumbagua Mtu Mwenye Ulemavu.

45. Kumdhalilisha au kumkandamiza Mtu Mwenye Ulemavu.

46. Kumtelekeza au kumkataa Mtu Mwenye Ulemavu.

47. Kukataa kumuajiri Mtu Mwenye Ulemavu.

48. Adhabu ya Jumla.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO


49. Maelekezo ya Waziri.

50. Kuzuia ulemavu.

51. Adhabu kwa Mtu Mwenye Ulemavu.

52. Kanuni.

53. Kufuta na kubakiza.

**Jadweli**

**SHERIA NAM. 8 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

22 Disemba, 2022

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU (HAKI NA FURSA) NAM. 9 YA MWAKA 2006 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA MASHARTI YANAYOHUSIANA NA WATU WENYE ULEMAVU NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, 2022 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti.

Ufafanuzi.

**2**. Katika Sheria hii isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"kumficha Mtu Mwenye Ulemavu" maana yake ni kumuweka au kumfungia ndani Mtu Mwenye Ulemavu kwa madhumuni ya kumtenganisha na jamii kwa kuhofia aibu au kwa sababu nyengine yoyote ambayo ni kinyume na sheria ambapo kutampelekea mtu huyo kukosa haki au fursa anazostahiki;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar lililoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Ulemavu" maana yake ni upungufu wa uwezo wa viungo vya mwili, akili au hisi unaomsababishia mtu kushindwa kumudu mazingira yake au kushiriki kikamalifu katika shughuli za kijamii;

"Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya" maana yake ni Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya lililoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Kumbagua Mtu Mwenye Ulemavu" maana yake ni kumfanyia Mtu Mwenye Ulemavu kitendo tofauti na mwengine kwa njia ya kumtenga au kumuwekea kizuizi kutokana na ulemavu alionao kwa madhumuni ya kumuathiri, kumdhoofisha au kubatilisha utambulisho, haki, fursa au hadhi yake;

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Katibu Mtendaji wa Baraza anayeteuliwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar ulioanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Ukondoeshaji" maana yake ni kuzingatia masuala ya ulemavu katika utekelezaji wa mipango ya kisekta ili kufikia ujumuishi wa Watu Wenye Ulemavu;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayeshughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

"Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu" maana yake ni jumuiya iliyoundwa na Watu wenye Ulemavu au kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu;

"Mtu Mwenye Ulemavu" maana yake ni mtu mwenye upungufu wa uwezo wa viungo vya mwili, akili au hisi unaomsababishia mtu kushindwa kumudu mazingira yake au kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Hifadhi" maana yake ni matunzo pamoja na huduma nyengine wanazopatiwa Watu Wenye Ulemavu.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI, USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA BARAZA

Uanzishwaji wa Baraza.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar.

(2) Baraza litakuwa ni chombo cha Serikali kisichojitegemea kikamilifu na kwa kutumia jina lake litakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kununua, kumiliki na kuondosha mali yoyote ya Baraza inayohamishika au isiyohamishika; na

(b) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo Baraza kwa asili yake linaweza kulitekeleza kwa mujibu wa Sheria hii.

Muhuri na Nembo ya Baraza.

**4.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Baraza katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Baraza.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Baraza katika waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Katibu Mtendaji.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Baraza utawekwa muhuri wa Baraza na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Muundo wa Baraza.

**5.**-(1) Baraza litaundwa na:

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais;

(b) Katibu Mkuu kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

(c) Katibu Mkuu kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya elimu;

(d) Katibu Mkuu kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya afya;

(e) Katibu Mkuu kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya usafiri barabarani;

(f) Mwenyekiti wa Jumuiya Mwamvuli ya Kitaifa ya Watu Wenye Ulemavu;

(g) mjumbe mmoja ambaye ni mwanafunzi mwenye Ulemavu kutoka katika jumuiya ya wanafunzi wenye Ulemavu iliyosajiliwa Zanzibar au kutoka katika moja ya Taaasi ya Elimu ya juu iliyopo Zanzibar inayotambuliwa na Serikali;

(h) wajumbe wasiozidi watatu kutoka katika Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu zenye uwakilishi nchi nzima kulingana na aina ya ulemavu; na

(i) wajumbe wawili kutoka sekta binafsi.

(2) Wajumbe chini ya aya za (h) na (i) za kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri kwa kuzingatia uzoefu, ujuzi, weledi, uadilifu na jinsia baada ya kushauriana na taasisi husika.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa Katibu wa Baraza.

"Kwa madhumuni ya kifungu hiki Jumuiya Mwamvuli" maana yake ni muungano wa hiyari wa jumuia za Watu Wenye Ulemavu au kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria za Zanzibar".

Kazi za Baraza.

**6**. Baraza litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia, kuratibu na kutekeleza masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

(b) kulinda, kuendeleza na kutetea haki na fursa za Watu Wenye Ulemavu;

(c) kuimarisha mashirikiano na kukuza mtandao na watu binafsi, taasisi za ndani na za kimataifa katika kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu;

(d) kwa kushirikiana na Wizara inayohusiana na elimu, kutoa miongozo juu ya matumizi na mafunzo ya lugha za alama na lugha nyengine zinazotumiwa na Watu Wenye Ulemavu;

(e) kufanya au kushajihisha utafiti unaohusiana na masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

(f) kuweka utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya;

(g) kutafuta fedha kwa ajili ya maendeleo ya Mfuko;

(h) kusimamia utekelezaji wa Mfuko; na

(i) kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Sheria hii.

Uwezo wa Baraza.

**7**. Baraza litakuwa na uwezo wa:

(a) kuingia au kusababisha kuingia katika maeneo ya umma, vyombo vya usafiri wa umma na sehemu nyengine kwa ajili ya kufanya ukaguzi kuhusiana na utekelezaji wa masharti ya Sheria hii;

(b) kwa kushirikiana na mamlaka husika, kuzuia au kusababisha kuzuiliwa jambo lolote linalovunja au linaloashiria kuvunja haki za msingi za Watu Wenye Ulemavu;

(c) kwa kushirikiana na mamlaka husika, kuichukulia hatua au kusababisha kuchukuliwa hatua kwa taasisi au mtu yeyote anayekiuka masharti ya Sheria hii;

(d) kusababisha kufanyiwa mapitio au marekebisho ya Sera au Sheria zinazosimamiwa na Sekta mbali mbali zinazokwenda kinyume na masharti ya Sheria hii; na

(e) kuchukua hatua nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Sheria hii.

Sifa za Mwenyekiti.

**8**. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ni Mtu Mwenye Ulemavu;

(c) ana angalau elimu ya sekondari;

(d) ana uzoefu angalau wa miaka mitano katika masuala ya Watu Wenye Ulemavu na haki za binaadamu; na

(e) ana kiwango cha juu cha uadilifu.

Makamu Mwenyekiti.

**9**. Wajumbe wa Baraza watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti.

Posho la wajumbe.

**10**. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Baraza watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyengine zinazohusika.

Kamati za Baraza.

**11**. Baraza linaweza kuanzisha Kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi mahsusi kama litakavyoona inafaa.

Muda wa wajumbe wa Baraza.

**12**. Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Baraza watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Kusita kuwa Mjumbe.

**13**. Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Baraza bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) kusitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Baraza;

(e) ikiwa mjumbe atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza; au

(f) kifo.

Kukasimu kazi za Baraza.

**14**.-(1) Baraza linaweza, linapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Katibu Mtendaji au Kamati ya Baraza.

(2) Endapo Baraza litakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

Mwenendo wa Baraza.

**15**. Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Baraza yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

**16**.-(1) Litaanzishwa Baraza la Watu Wenye Ulemavu katika kila wilaya litakalojulikana kama Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

(2) Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya litaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Mkuu wa Wilaya kutoka miongoni mwa Wenyeviti wa Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu katika wilaya;

(b) mjumbe mmoja kutoka sekta binafsi;

(c) Wenyeviti wa Jumuiya tatu za Watu Wenye Ulemavu zilizopo katika wilaya; na

(d) Maafisa wawili kutoka sekta ya elimu na afya wa wilaya.

(3) Wajumbe chini ya aya za (b), (c) na (d) za kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, watateuliwa na Mkuu wa Wilaya kwa kuzingatia uzoefu, ujuzi, weledi, uadilifu na jinsia.

(4) Afisa wa masuala ya Watu Wenye Ulemavu wa wilaya atakuwa Katibu wa Baraza la Watu wenye Ulemavu la Wilaya.

Muda wa wajumbe wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

**17**. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Kazi za Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

**18**.-(1) Kazi za Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya zitakuwa:

(a) kuratibu na kutekeleza masuala ya Watu Wenye Ulemavu katika ngazi ya wilaya;

(b) kuwatambua Watu Wenye Ulemavu na mahitaji yao,

(c) kuhakikisha masuala ya Watu Wenye Ulemavu yanajumuishwa katika mipango, programu za maendeleo na shughuli zinazotekelezwa katika ngazi za wilaya; na

(d) kutoa elimu juu ya masuala ya Watu Wenye Ulemavu.

(2) Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya litawasilisha mipango na ripoti za utekelezaji wa shughuli zake kwa Baraza kwa kila robo mwaka.

Mwenendo wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya.

**19**.-(1) Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya litajiwekea utaratibu wake wenyewe wa vikao.

(2) Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya litakutana mara moja kila robo mwaka.

Katibu Mtendaji wa Baraza.

**20.**-(1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji wa Baraza atakayeteuliwa na Rais.

(2) Katibu Mtendaji atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu na Afisa Masuuli wa Baraza.

Sifa za Katibu Mtendaji.

**21.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali;

(c) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Katibu Mtendaji.

**22.** Kazi za Katibu Mtendaji wa Baraza zitakuwa:

(a) kutekeleza shughuli za kila siku za Baraza;

(b) kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Baraza;

(c) kusimamia utekelezaji wa Sera za Taifa, Sheria na Miongozo mbali mbali inayohusiana na masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

(d) kusajili na kuweka taarifa za Watu Wenye Ulemavu;

(e) kuzitambua na kuweka taarifa za Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu zilizosajiliwa Zanzibar;

(f) kuimarisha mashirikiano ya kisekta, kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusiana na masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

(g) kusimamia utekelezaji wa vipengele vya sera na mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusiana na masuala ya Watu Wenye Ulemavu ambayo Tanzania imeiridhia; na

(h) kutekeleza kazi nyengine yoyote iliyoelezwa katika Sheria hii.

Sekretarieti.

**23**.-(1) Kutakuwa na Sekeretarieti ya Baraza inayoundwa na Wakuu wa Idara, Divisheni na Vitengo ambayo itaongozwa na Katibu Mtendaji na itakuwa na jukumu la kutekeleza shughuli za kila siku za Baraza zikiwemo:

(a) kutekeleza shughuli za kiuendeshaji za Baraza;

(b) kuandaa mipango ya utekelezaji ya maamuzi ya Baraza;

(c) kutayarisha na kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza;

(d) kuandaa ripoti; na

(e) kutekeleza kazi nyengine yoyote kama itavyoelekezwa na Baraza chini ya masharti ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza litaanzisha Idara, Divisheni na Vitengo kama litakavyoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Wakuu wa Idara watateuliwa na Baraza kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa Vitengo na Divisheni watateuliwa na Katibu Mtendaji kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(5) Wakuu wa Idara, Divisheni na Vitengo watawajibika kwa Katibu Mtendaji.

Wafanyakazi wa Baraza.

**24**. Kutakuwa na wafanyakazi wa Baraza watakaoajiriwa kwa kuzingatia vigezo na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

## SEHEMU YA TATU
## USAJILI WA WATU MWENYE ULEMAVU NA KUZITAMBUA JUMUIYA ZA WATU WENYE ULEMAVU

Taratibu za usajili.

**25**.-(1) Mtu yeyote mwenye ulemavu atasajiliwa na Katibu Mtendaji kwa mujibu wa kanuni.

(2) Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, watu wataotaka kusajili Jumuiya inayohusiana na Watu Wenye Ulemavu wanatakiwa kupata barua ya mapendekezo kutoka Baraza kabla ya kusajiliwa kama Jumuiya Isiyo ya Kiserikali.

Daftari la kumbukumbu.

**26.**-(1) Baraza litaanzisha Daftari la Kumbukumbu litakaloweka taarifa za Watu Wenye Ulemavu na Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu.

(2) Daftari la kumbukumbu litakuwa chini ya uangalizi wa Katibu Mtendaji.

Sifa za Kusajiliwa.

**27.**-(1) Mtu mwenye Ulemavu atalazimika kusajiliwa ikiwa amezaliwa au anaishi Zanzibar.

(2) Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu inayoomba kutambuliwa itatakiwa:

(a) kuwa na cheti halali cha usajili wa asasi za kiraia; na

(b) iwe inajishughulisha na masuala ya Watu Wenye Ulemavu ndani ya Zanzibar.

## SEHEMU YA NNE
## HAKI NA FURSA

Haki na fursa.

**28.**-(1) Watu Wenye Ulemavu wanastahiki haki zote za msingi za binadamu sawa na watu wengine ikijumuisha:

(a) haki ya elimu ikijumuisha mafunzo ya amali na mafunzo ya kukabiliana na maisha kulingana na aina za ulemavu;

(b) haki ya kufanya kazi na ajira;

(c) haki ya kupata huduma za afya zikiwemo matibabu, matengenezo na marekebisho yanayohusiana na ulemavu;

(d) haki ya kupata habari na mawasiliano kwa kuzingatia aina za ulemavu;

(e) haki ya kuishi kwa kujitegemea na kujumuishwa katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kisiasa; na

(f) haki ya kushiriki katika michezo na burudani.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1)(a) cha kifungu hiki, Baraza kwa kushirikiana na taasisi yenye dhamana na masuala ya elimu litahakikisha:

(a) Watu Wenye Ulemavu wanapata elimu na mafunzo ya amali katika ngazi zote; na

(b) kuwepo na mfumo wa elimu jumuishi unaozingatia mahitaji maalum ya Watu Wenye Ulemavu katika ngazi zote za elimu.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, taasisi zenye dhamana ya kazi na utumishi wa umma zitahakikisha kuwa zinatoa kipaumbele na mazingatio kwa nafasi za ajira zinazotolewa katika sekta ya umma na sekta binafsi kwa Watu Wenye Ulemavu.

(4) Wizara na taasisi zinazohusika na masuala ya kazi na ajira zitahakikisha zinaweka mazingira yanayowawezesha Watu Wenye Ulemavu kuajiriwa, kujiajiri au kushiriki katika ushindani wa soko la ajira kitaifa, kikanda na kimataifa.

(5) Kila muajiri atahakikisha anaweka mazingira wezeshi kwa Watu Wenye Ulemavu kufanya kazi kwa kujitegemea.

(6) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1)(c) cha kifungu hiki, Taasisi yenye dhamana ya masuala ya afya itahakikisha upatikanaji wa huduma maalum za afya zinazohitajiwa na Watu Wenye Ulemavu.

(7) Wizara na taasisi zenye dhamana ya usimamizi wa masuala ya habari zitahakikisha zinazingatia masuala ya Watu Wenye Ulemavu katika kupata habari.

(8) Taasisi au mtu yeyote atakayevunja haki za Watu Wenye Ulemavu atachukuliwa hatua kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote inayohusika.

(9) Watu Wenye Ulemavu watapatiwa fursa zitakazowawezesha kufikia na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii bila ya utegemezi zikiwemo fursa za ajira, elimu ya juu na uwezeshaji kiuchumi.

Ufikiaji.

29.-(1) Baraza litashajihisha ufikiaji wa miundombinu ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, afya, elimu, habari na mawasiliano ili kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kufaidika kikamilifu na haki zote za binaadamu kwa kujitegemea.

(2) Katika kuhakikisha ufikiaji wa habari na mawasiliano, Baraza litashajihisha matumizi ya lugha za alama, nukta nundu, miundo au lugha nyengine zinazoweza kufikiwa na kutumika kwa mawasiliano ya Watu Wenye Ulemavu na matumizi ya teknolojia ya vifaa saidizi vya mawasiliano.

Wajibu wa kulinda haki za Watu Wenye Ulemavu.

**30**. Kila mtu ana wajibu wa kutekeleza, kulinda na kutetea haki za Watu Wenye Ulemavu ikijumuisha kutoa taarifa zinazohusiana na uvunjwaji wa haki hizi.

Kuondoa Ubaguzi na udhalilishaji.

**31**.-(1) Watu Wenye Ulemavu hawatobaguliwa au kudhalilishwa kwa namna yoyote ile na katika ngazi zote kutokana na sababu ya ulemavu wao.

(2) Baraza litaanzisha programu mbali mbali kuzuia Watu Wenye Ulemavu kubaguliwa au kudhalilishwa ikijumuisha kuitwa majina yasiyofaa, kudharauliwa, kukejeliwa, kutumiwa vibaya kupitia mitandao ya kijamii, kupigwa na kudhalilishwa kijinsia.

## SEHEMU YA TANO
## UKONDOESHAJI NA UJUMUISHAJI

Ukondoeshaji na ujumuishaji.

**32**.-(1) Taasisi yoyote ya umma au binafsi itahakikisha:

(a) inakondoesha na kujumuisha masuala au mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu katika sera, sheria, miongozo, mipango na mifumo ya utekelezaji wa shughuli zake;

(b) huduma wanazozitoa zinawafikia Watu Wenye Ulemavu;

(c) kuwepo kwa huduma za ziada kwa Watu Wenye Ulemavu katika maeneo ya kazi; na

(d) taratibu za utoaji na upatikanaji wa huduma zinazozingatia mahitaji maalum ya Watu Wenye Ulemavu.

(2) Baraza litasimamia na kutoa miongozo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa masuala ya Watu Wenye Ulemavu katika ngazi zote.

Miundombinu Rafiki.

**33**.-(1) Baraza litashajihisha uwekaji wa miundombinu rafiki katika maeneo yote hasa yanayotumiwa na umma ikiwemo maeneo ya usafiri wa barabarani, anga na baharini, michezo burudani na kumbi za mikutano.

(2) Wizara na taasisi zenye dhamana ya masuala ya ujenzi zitahakikisha vibali vya ujenzi vinatolewa baada ya usanifu wa majengo kwa kuzingatia miongozo ya miundombinu rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu.

## SEHEMU YA SITA
## MFUKO WA MAENDELEO WA WATU WENYE ULEMAVU

Mfuko wa Maendeleo wa Watu Wenye Ulemavu.

**34.** Kunaanzishwa Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Maendeleo wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar.

Uendeshaji na Usimamizi wa Mfuko.

**35.** Mfuko utaendeshwa na Katibu Mtendaji na kusimamiwa na Baraza chini ya masharti ya Sheria na taratibu za Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Vyanzo vya Mfuko.

**36.** Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitakuwa:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) misaada halali, michango ya hiari au michango mengine yoyote ambayo Baraza linaweza kupokea kwa madhumuni ya Mfuko;

(c) fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo; na

(d) fedha zinazotokana na shughuli za uchangishaji wa fedha zinazofanywa na Baraza kwa ajili ya maendeleo ya Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu.

Malengo ya Mfuko.

**37.** Malengo ya Mfuko ni kuhakikisha upatikanaji, uimarishaji, uwezeshaji na ustawi wa Watu Wenye Ulemavu ambayo yanajumuisha:

(a) kutoa au kuchangia gharama za huduma zikijumuisha vifaa saidizi, matibabu, marekebisho, elimu na mafunzo ya amali, matunzo na huduma nyengine kama zitakavyohitajika kwa kuzingatia taratibu zitakazowekwa na Baraza;

(b) kuwajengea uwezo Watu Wenye Ulemavu na Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu; na

(c) kusaidia juhudi zinazofanywa na Watu Wenye Ulemavu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya Watu Wenye Ulemavu.

Ukaguzi wa Mfuko.

**38.** Mfuko utakaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine zozote zinazohusika.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya Fedha.

**39**. -(1) Fedha na rasilimali za Baraza zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi; na

(b) ruzuku halali, zawadi, msaada au michango kama Baraza litakavyoweza kupokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote.

(2) Miamala yote ya fedha ya Baraza itafanywa na itaongozwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine yoyote inayohusika.

Bajeti ya Baraza.

**40**. -(1) Katibu Mtendaji, kila mwaka wa fedha, atawasilisha katika Baraza kwa ajili ya majadiliano na kuidhinisha juu ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi ya Baraza kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Makadirio ya mapato na matumizi ya Baraza yataandaliwa kwa mujibu wa matakwa na masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na miongozo mengine yoyote inayoweza kutolewa na Serikali mara kwa mara.

Hesabu na Ukaguzi.

**41**.-(1) Baraza litaweka na kutunza kumbukumbu sahihi ya vitabu vya hesabu.

(2) Taarifa za fedha za mwaka zitakaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine husika za fedha.

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Kumficha Mtu Mwenye Ulemavu.

**42**. Mtu yeyote atakayemficha mtu mwenye ulemavu atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Elfu Hamsini za Tanzania na isiyozidi Shilingi Laki Tano za Tanzania.

Taarifa ya Uongo.

**43**. Endapo mtu atatoa taarifa ya uongo kwa madhumuni ya kusajiliwa au kupata fursa za Mtu mwenye Ulemavu, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Tanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tatu za Tanzania au kifungo kwa kipindi cha miezi sita au vyote viwili.

Kumbagua Mtu Mwenye Ulemavu.

**44**. Endapo mtu anambagua Mtu Mwenye Ulemavu kutokana na ulemavu wake, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Tanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tano za Tanzania.

Kumdhalilisha au kumkandamiza Mtu Mwenye Ulemavu.

**45**. Mtu yeyote anayemdhalilisha au kumkandamiza Mtu Mwenye Ulemavu kwa:

(a) kumwita jina lisilofaa kutokana na aina ya ulemavu wake;

(b) kumuigiza kwa matamshi, mwendo au ishara kutokana na hali ya ulemavu wake;

(c) kumdharau au kumkejeli kwa sababu ya ulemavu wake;

(d) kumtumia kupitia mitandao ya kijamii kwa madhumuni ya kumdhalilisha, kuburudisha au vyenginevyo;

(e) kumtumia kama njia ya kujipatia kipato;

(f) kumfanyisha kazi ya kujipatia kipato bila kumlipa ujira anaostahiki; au

(g) kufanya jambo jengine lolote kwa madhumuni ya kumdhalilisha,

atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja za Tanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Moja za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi miwili au vyote viwili.

Kumtelekeza au kumkataa Mtu Mwenye Ulemavu.

**46**. Mtu yeyote mwenye jukumu la kumtunza Mtu Mwenye Ulemavu ikiwa atamtelekeza au kumkataa kwa namna yoyote ile, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Tanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tatu za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote viwili.

Kukataa kumuajiri Mtu Mwenye Ulemavu.

**47**. Mtu yeyote atakayekataa kumuajiri Mtu Mwenye Ulemavu kutokana na ulemavu wake kinyume na masharti ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu za Tanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tano za Tanzania.

Adhabu ya Jumla.

**48**. Taasisi au mtu yeyote aliyevunja sharti lolote chini ya Sheria hii ambapo hakuna adhabu makhsusi iliyotolewa, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili za Tanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Mbili za Tanzania.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Maelekezo ya Waziri.

**49**. Waziri anaweza kutoa maelekezo kwa Baraza kwa maandishi juu ya utekelezaji wa kazi za Baraza, na Baraza litatekeleza maelekezo hayo kwa mujibu wa Sheria hii.

Kuzuia ulemavu.

**50**. Serikali kupitia taasisi zake mbali mbali itasimamia na kuchukua hatua za kuzuia ulemavu unaosababishwa na:

(a) ajali za barabarani;

(b) maradhi na sababu nyengine za kiafya;

(c) ajali, maradhi na majanga yanayotokana na kazi; na

(d) mambo mengine yanayosababisha matukio ya ulemavu.

Adhabu kwa Mtu Mwenye Ulemavu.

**51**. Endapo Mtu Mwenye Ulemavu atatiwa hatiani kwa kosa lolote kwa mujibu wa sheria husika na kuhukumiwa kutumikia Chuo cha Mafunzo, adhabu atakayopangiwa ilingane na hali na aina ya ulemavu wake.

Kanuni.

**52**. Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii, uendeshaji na usimamizi wa jumla wa Baraza.

Kufuta na kubakiza.

**53**.-(1) Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa), Nam. 9 ya Mwaka 2006 inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) kitu chochote kilichofanywa au kingepaswa kufanywa chini ya Sheria iliyofutwa, isipokuwa kwa kiwango ambacho hakipingani na Sheria hii, kitaendelea kuwa halali na kitachukuliwa kuwa kimefanywa chini ya Sheria hii; na

(b) kitu chochote kilichoanzishwa katika Sheria iliyofutwa ambacho bado hakijakamilika isipokuwa kwa kiwango ambacho hakipingani na Sheria hii, kitakamilishwa na kuchukuliwa kuwa chini ya Sheria hii.

## JADWELI
## MWENENDO WA BARAZA

(Chini ya kifungu cha 15)

---

Vikao vya Baraza.

**1.**-(1) Baraza litakutana kila robo mwaka na linaweza kukutana katika vikao vya dharura muda wowote inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, vikao vya dharura havitazidi vikao vya kawaida kwa mwaka.

(3) Vikao vyote vya Baraza vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Baraza na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**2.** Akidi katika vikao vyote vya Baraza itakuwa ni zaidi ya nusu ya wajumbe wake.

Maamuzi ya Baraza.

**3.** Maamuzi ya Baraza yatafanywa kwa maafikiano, ikiwa hakuna maafikiano, maamuzi yatafanywa kwa kura na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Taratibu za vikao.

**4.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Baraza litakuwa na uwezo wa kusimamia taratibu zake zenyewe kuhusiana na vikao na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake ikijumuisha Kamati za Baraza.

Mjumbe mualikwa.

**5.** Baraza linaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe kuhudhuria katika majadiliano ya vikao vya Baraza kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kubainisha maslahi.

**6.**-(1) Mjumbe wa Baraza ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Baraza, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni wa kikao cha Baraza.

(2) Ubainishaji wa maslahi utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Baraza katika kufanya maamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya maamuzi.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 23 Novemba, 2022.

.............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***